

Kuishi Maisha Yanayompendeza Mungu (Sehemu ya 1)

Inategemea sura ya 12 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kinachopatikana kwenye jw.org/sw.

LENGO: Chunguza mambo unayoamini na sababu za kuamini mambo hayo, chunguza kile ambacho Biblia inafundisha, na uone jinsi unavyoweza kuwaeleza wengine mambo unayoamini.



JE, UNaweza KUWA RAFIKI YA MUNGU?

1 CHUNGUZA MAMBO UNAYOAMINI

Kwa nini huenda watu wengine wakasema hapana?

Kwa nini huenda wengine wakasema ndiyo?

Wewe unaamini nini?

Kwa nini unaamini hivyo?

2

CHUNGUZA KILE AMBACHO BIBLIA INAFUNDISHA

Wanadamu waaminifu katika nyakati za Biblia walikuwa rafiki za Mungu.

(Ona sura ya 12 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 1-3.)

Soma Danieli 9:23, Matendo 13:22, na Yakobo 2:23.

Taja wanadamu watatu ambao Mungu aliwaona kuwa rafiki zake.

Soma Mwanzo 22:18.

Kwa nini Mungu aliwaona watu hao kuwa rafiki zake? (Dokezo: Ona Zaburi 25:14.)



Kama tu ambavyo marafiki wa kweli wanasaidiana wakati wa taabu, Yehova, Rafiki yetu wa karibu zaidi, yuko tayari kutusaidia tunapomhitaji

Yehova anawaimarisha rafiki zake ili wafanye yaliyo sawa.

(Ona sura ya 12 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 4-5.)

Soma 2 Mambo ya Nyakati 16:9.

Kulingana na mstari huu, Yehova anatamani kufanya nini?

Soma Zaburi 32:8 na 55:22.

Yehova anatumia njia gani mbili kuwasaidia rafiki zake?

Unahisije kujua kwamba Yehova anakualika kuwa rafiki yake?

3

ELEZA MAMBO UNAYOAMINI

MTU AKISEMA . . .

Kwa kuwa Mungu ni mweza yote, haiwezekani kwa wanadamu kumkaribia.

UNAWEZA KUSEMA HIVI . . .

Watu wengi wanaamini hivyo. Lakini mimi siamini hivyo kwa sababu . . .

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje kuelewa andiko hilo?

MTU AKISEMA . . .

Ni watu wa pekee sana wanaoweza kuwa rafiki za Mungu.

UNAWEZA KUMJIBU HIVI . . .

Ni kweli kwamba Biblia inaeleza kuhusu mambo fulani ya pekee ambayo baadhi ya rafiki za Mungu wametimiza. Lakini ninaamini kwamba mtu yeyote anaweza kuwa rafiki ya Mungu kwa sababu . . .

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje kuelewa andiko hilo?
